JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA MTWARA

TAARIFA YA HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA WA MTWARA LIGULA

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa
S.L.P. 520
Simu/Fax Na.023-2333194
Barua Pepe: afya@mtwara .go.tz
Tovuti: www.mtwara.go.tz

UTANGULIZI

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mtwara (Ligula) ilifunguliwa rasmi tarehe 14/10/1964 na Rais wa kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Hospitali hii ilianza na majengo machache yaliyokuwa karibu na mapokezi ya sasa. Wodi ya zamani ya wazazi "Frelimo" ilikuwa ni hospitali ya majeruhi wa chama cha Frelimo ikijulikana kwa jina la "Americo Boavida Hospital". Kwa sasa wodi hii inafanyiwa ukarabati kwa kushirikiana na Chuo cha Uuguzi Mtwara kutokana na ubovu wa jingo, hivyo jengo jipya la wodi ya wazazi lililojengwa kwa msaada wa shirika la maendeleo la ujerumani (GIZ) ndio linatumia kwa huduma za uzazi.

Hospitali hii inahudumia kama hospitali ya wilaya kwa wakazi wa Manispaa ya Mtwara Mikindani, Mtwara Vijijini, baadhi ya wakazi wa mkoa wa Lindi (vijiji vya kuanzia Mingoyo kuja hadi Mtwara), wakazi wa nchi jirani ya Msumbiji (vijiji vilivyo mpakani na Tanzania) na inahudumia kama hospitali ya Rufaa kwa hospitali zote za mkoa wa Mtwara ambao jumla ya wakazi wake ni 1,323,568. Kwa sasa hospitali inauwezo wa kuchukua vitanda 250 (bed capacity), kiwango cha matumizi ya vitanda (Bed occupancy rate ni 75%) na wastani wa wagonjwa wanaolazwa kukaa hospitalini (Average length of stay) ni siku 6 hadi siku 7.

HUDUMA ZINAZOTOLEWA

Hospitali kwa sasa inatoa huduma zifuatazo:

1. Huduma ya Wagonjwa wa Nje (Outpatient services)
2. Huduma ya Wagonjwa wa Ndani / Kulaza Wagonjwa (Inpatient services)
3. Huduma ya Maabara (Laboratory services)
4. Huduma ya Picha za Mionzi (X-Ray, Ultrasound, ECG)
5. Huduma ya Matibabu ya Macho na Miwani (Eye care services)
6. Huduma ya Matibabu ya Meno (Dental services)
7. Huduma za Afya ya Uzazi na Mtoto (Reproductive and Child Health services)
8. Huduma za Mapasuaji (Surgical services)

9. Huduma za ushauri nasaha na kupima virusi vya ukimwi (VCT servises)
10. Huduma za ushauri na uzuiaji wa maambukizi ya virusi vya ukimwi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto (PMTCT servises)
11. Huduma za utoaji wa dawa za kupunguza makali ya Ukimwi (CTC services)
12. Huduma ya Tiba ya Kifua Kikuu na Ukoma (TB and Leprosy)
13. Huduma shirikishi za Kifua Kikuu na Ukimwi (TB/HIV Intergration)
14. Huduma za Utafiti wa Kimatibabu (Research)

Mapema mwaka uliopita ujenzi wa majengo mawili ya Hospitali yamekamilika, Jengo la huduma za dharura na Jengo la kulaza wagonjwa wa daraja la kwanza (Grade One).

HALI YA VIFAA TIBA

Hospitali ina vifaa tiba ambavyo vinafanya kazi kama vile X-Ray, Utral Sound, Mashine za Maabara, mashine kwenye chumba cha upasuaji. Tatizo zinazozikabili hizi mashine ni pamoja na ukosefu wa pesa za matengenezo, kwani gharama za matengenezo ya hizi mashine ni kubwa kulinganisha na makusanyo ya hospitali.

TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA GIZ MKOA WA MTWARA

Wadau wa maendeleo wa shirika la GIZ wamekuwa ni msaada mkubwa sana katika utoaji wa huduma za Afya katika Mkoa wa Mtwara kwani kuna miradi mingi ambayo wameifanya katika Mkoa wa Mtwara na sasa hivi wanafanya shughuli zao katika maeneo yafuatayo katika kuboresha huduma ya mama na mtoto, maeneo hayo ni:-

- Kujengewa uwezo kwa watoa huduma wa Afya(Capacity Development For Hcw In EmONC)
- Usimamizi shirikishi na mafunzo elekezi(montoring and supportive 3
- Ufuatiliaji na tathimini ya upatikanaji wa takwimu sahii(monitoring and evaluation,data management)

- Mikakati ya kuwafanya watumishi waendelee kubakia kufanya kazi katika mpango wa kuboresha upatikanaji wa rasilimali watu(hr retention& needs based planning)
- Upatikanaji wa vifaa tiba na kufanyia ppm(availability of medical equipments)
- Kuimarisha mfumo wa rufaa kutoka zahanati,vituo vya afya ,hospitali za wilaya na mkoa(support to develop ment of functional referal system)
- Kuboresha utoaji wa huduma zenye ubora kwenye afya ya uzazi na watoto wachanga(qulity improvement in obstetrics and emoonc)

CHANGAMOTO

- Upungufu wa wafanyakazi kwa asilimia 44%. Hospitali ina jumla ya wafanyakazi wa afya 267 wa kada mbalimbali. Kwa mujibu wa Ikama ya Watumishi ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ya 2014-2018 hospitali ina uhaba wa wafanyakazi 211 kati ya 478 kiwango cha chini wanaohitajika kuwepo ili kutoa huduma kwa ngazi ya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa. Kutokana na upungufu huu hospitali haina Madaktari Bingwa wakutosha swala linalopelekea wagonjwa kupewa rufaa mara kwa mara.
- Upungufu wa fedha kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba.

- Miundombinu na majengo ya hospitali ni ya muda mrefu hivyo Kufanya miundombinu hiyo kuwa ni chakavu na inayohitaji ukarabati (jengo la kitengo cha wagonjwa wa nje (OPD), kitengo cha huduma za Afya ya Akili)

  Pia majengo haya ya hospitali yana nafasi ndogo hivyo kusababisha kushindikana kuhudumiwa kwa wagonjwa wengi kwa wakati mmoja.
  (Wodi ya Wazazi na Watoto).
  Majengo ambayo hayakidhi viwango kama chumba cha kuhifadhia maiti,
  Hospitali pia inahitaji kukamilika kwa ujenzi wa uzio unaozunguka hospitali.

- Kutokuwepo kwa gari la wagonjwa "ambulance" lenye nafasi ya kutosha na vifaa maalum vya kutolea huduma ya dharura kwa mgonjwa pamoja na bajeti finyu ya huduma za rufaa kwa wagonjwa wanaohitajika kupelekwa hospitali ya taifa ya Muhimbili. (Gari la wagonjwa lililopo linaufinyu wa nafasi hivyo kufanya utoaji wa huduma na uwekaji wa vifaa vya huduma ya dharura kupata changamoto ya nafasi.)

- Hospitali inakabiliwa na changamoto ya upungufu wa vifaa tiba vya utambuzi wa magonjwa mbalimbali (OGD, CT Scan), vifaa tiba kwa ajili ya kutolea huduma ya wagonjwa mahututi (ICU), vifaa tiba kwa ajili ya kutolea huduma ya Tiba ya mazoezi (Physiotherapy).

HATUA ZILIZOCHUKULIWA

- Ili kuhakikisha huduma zinaboreka zaidi Hospitali iliomba msaada Eco Bank kwa ukarabati wa Wodi ya Watoto

- Kwa kutumia vyanzo vya ndani, Hospitali imekamilisha ukarabati mdogo wa Wodi ya Wazazi na kuboresha huduma kwa watoto njiti.

- Tarehe 23 Novemba 2015 Katibu Tawala wa Mkoa aliunda kamati 10 ambazo zimepewa jukumu la kuainisha changamoto za hospitali na kupendekeza ufumbuzi wa changamoto hizo ikiwa ni pamoja na kuandaa Concept Note ambazo zitatumika kuombea msaada wa kifedha kwa wadau wa maendeleo na serikali kuu.

- Mwezi Julai 2015 Hospitali kwa kushirikiana na shirika la maendeleo la Kibaha ilifunga mfumo wa ki-elekroniki wa huduma za ukusanyaji mapato ambao mpaka sasa unasaidia kuimarisha uwezo wa ukusanyaji mapato kwa uhakika na kutumia mapato hayo kuboresha huduma za Hospitali

- Kwa kushirikiana na makampuni ya gesi Mkoani, Hospitali imeweza kufanya harambee na kukusanya fedha ambazo zimetumika kununua vifaa kwa

kitengo cha magonjwa ya dharura. Asilimia kubwa ya vifaa vinavyotumika katika kitengo hiki vimepatikana katika msaada huu.

- Kupitia ofisi ya Mbunge wa jimbo la Mtwara Mjini kumeweza kufanyika ujenzi wa awali wa jengo la kusubiria ndugu wa wagonjwa, ujenzi huo bado haujakamilika.

- Kupitia ufadhili wa Taasisi ya Heart to Heart Foundation na Shirika la Maendeleo nchini Korea Kusini (KOICA) jengo la idara ya Macho limefanyiwa ukarabati na upanuzi mkubwa pamoja na ujenzi wa chumba cha mapasuaji ya macho na pia kupitia taasisi hiyo hiyo hospitali imepata vifaa tiba mbalimbali kwa ajili ya huduma ya macho kwa kiasi cha USD 130,000/= .

- Kupitia Mradi wa uboreshaji wa Afya ya Mama na Mtoto (IMCH) ulioko chini ya ufadhili wa GIZ na VSO tunategemea kupokea mashine ndogo ya Ultrasound pia kuboresha kitengo cha matengenezo ya vifaa tiba vya hospitali kwa kuwapatia mafunzo mafundi husika wa vifaa tiba hivyo.

- Kupitia Mfuko wa Taifa Bima ya Afya (NHIF) hospitali iko katika hatua za kupata mkopo wa kuiwezesha kupata kifaa cha mashine ya Ultrasound (convex probe) ili kuiwezesha mashine hiyo ya Ultrasound ifanye kazi.

MAONI YA KUBORESHA HUDUMA ZA HOSPITALI

- Kutoa kipaumbele kwa bajeti ya Hospitali ili iweze kupatikana kwa wakati na kukidhi mahitaji wa uendeshaji wa hospitali kwa kununua madawa, vifaa tiba, ukarabati na huduma kwa watumishi.

- Kusaidia hospitali kupitia viongozi wa siasa, jamii na taasisi za kidini katika kuwaelimisha wananchi wa Mtwara kutumia vituo vingine vya afya na zahanati kwa magonjwa yanayoweza kutibika katika vituo hivyo ili kupunguza msongamano wa wagonjwa hospitalini. Hii itasaidia kupunguza

msongamano na kutoa kwa ubora huduma za rufaa zilizolengwa kwa hospitali ya rufaa kwa wakati.

- Kufanya jitihada za makusudi za kuisaidia Hospitali iweze kupata wataalamu wa kada muhimu kama Madaktari Bingwa, Madaktari, wauguzi, Wataalamu wa Maabara na Wataaalamu wa Huduma za Mionzi.

- Pia kufanya juhudi za makusudi kusaidia upatikanaji wa nyumba kwa ajili ya makazi ya watumishi wa hospitali hususani wataalamu wa kada muhimu.

HITIMISHO

Uongozi wa Hospitali na Seksheni ya Afya, Ustawi wa Jamii, na Lishe inapenda kutoa shukrani kwako wewe Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kutembelea hospital yetu hii ya Ligula.

Pili tunapenda kutoa shukrani za dhati kwa Mh. Mkuu wa Mkoa kwa kuweka kipaumbele katika kuboresha huduma zinazotolewa hapa Hospitali ili ziweze kuwa na ubora unaokusudiwa.

Tatu tunapenda kumshukuru Katibu Tawala Mkoa pamoja na timu nzima ya Sekretarieti ya Mkoa kwa kutenga muda mahsusi wa kutafakari kwa pamoja changamoto za Hospitali na kupanga namna ya kuzitatua kwa kutumia ubunifu wa kitaaluma na mikakati ya kutatua changamoto za Hospitali.

Pia uongozi unapenda kuwashukuru watumishi wote ambao wamekuwa wakiendelea kutoa huduma za afya bila kuchoka na katika mazingira ambayo yanakabiliwa na changamoto mbalimbali.

Kazi ya kuboresha afya na kuokoa maisha ya wananchi wa Mtwara ipo mikononi mwetu na tujitahidi kwa kila hali kuhakikisha kuwa tunatekeleza wajibu wetu.

Daktari kiongozi hatua za utekelezaji wa mikakati ya kukabiliana na changamoto zinazoikabili Hospitali ya Rufaa ya Ligula ipo kwenye kiambatanisho.

Naomba kuwasilisha.

Dr.Wedson Sichalwe
MGANGA MKUU WA MKOA
MTWARA